ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Arubaini - Tarehe 6 Agosti, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mtakumbuka kwamba hivi karibuni tarehe siikumbuki sawa sawa lakini kwenye mwezi wa saba uliopita, tulipata ujumbe kutoka Bunge la Oman wanaita Majles A'Shura, ambao ulifikia hapa Tanzania pamoja na shughuli nyengine pale Tanzania Bara, lakini hatimaye walipata nafasi pia wakaja hapa Zanzibar. Ulikuwa ni ujumbe wa Bunge, jumla yao 17 na Katibu.

Ujumbe huo uliongozwa na Mhe. Spika wa Bunge hilo la Oman, tukafanya mazungumzo marefu kidogo lakini hatimaye baada ya kurudi nyumbani wakaleta barua rasmi kutoa pongezi kwa mapokezi. Vile vile kwa mazungumzo ambayo yalikuwa ni mazuri. kwa hivyo naomba nichukue nafasi hii kutoa tarifa ya pongezi waliyotuletea ambayo imetumwa kupitia kwangu ili niwape Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwangu pongezi zetu tulizopewa na Mhe. Spika wa Bunge la Oman. Barua inajieleza kama ifuatavyo:-

Honourable Pandu Ameir Kificho,
Speaker,
Parliament of Zanzibar,
United Republic of Tanzania.

Your Excellency,

I would like to express my profound gratitude and appreciation to the warm and great hospitality accords to me and the accompanying delegation during our visit to the United Republic of Tanzania, which has a reflected the cordial relations that bind the Omani and Tanzanian people, and confirmed the depth of the consolidated bonds based on fraternity and affinity. I wish Your Excellency and the friendly people of Tanzania further progress and prosperity.

Please accept your Excellency the assurance of the highest consideration.

Khalid bin Hilal Al Maawali,
Chairman of Majlis A'shura

Barua hii imeandikwa na Mhe. Khalid bin Hilal Al Maawali, *Chairman of Majlis A'shura* ya Oman. Naomba kuwasilisha kwenu salamu hizi za pongezi ambazo Mwenyekiti wa Bunge hilo ametuletea kwa ajili yetu. Naomba kuwasilisha salamu hizo. Ahsante sana.(*Makofi*).

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kuandika Sheria Inayohusiana na Makampuni na Jumuia Nyengine na Kuweka Masharti Madhubuti Zaidi ya Uratibu na Udhibiti wa Kampuni, Jumuia na mambo yanayohusina na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mezani Mswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria Mbali Mbali za Ardhi na mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kufuta na kuna Sheria ya Biashara ya Zanzibar Nam. 4 ya mwaka 1989 na kuweka vifungu vya kuimarisha Biashara Zanzibar na Mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika, kwa idhini yako pia naomba kuwasilisha kwenye Baraza lako Tukufu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara na Mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe na Waheshimiwa Mawaziri kabla sijawakaribisha Mawaziri ambao wanataka kutoa hoja ya kusomwa mswada kwa mara ya kwanza labda nieleze jambo moja dogo tu kuhusu utaratibu. Tunapowasilisha miswada hii kusomwa kwa mara ya Kwanza tunachotakiwa tukiseme Waheshimiwa Mawaziri ni Kusoma yale maelezo marefu ya Mswada huu na kumalizia kwa kusema naomba kusomwa kwa mara ya kwanza. Twende kwa utaratibu huo ili ifahamike huo Mswada wenyewe ni hasa upi unaowekwa mbele ya Baraza hili kwa kusomwa kwa mara ya kwanza.

Bada ya hayo, basi naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kuandika Sheria Inayohusu Kampuni na Jumuia nyengine Kuweka masharti madhubuti zaidi ya uratibu na udhibiti wa Kampuni, Jumuia na mambo yanayohusiana na hayo. Sasa naomba Usomwe Kwa Mara ya Mwanzo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba sasa Mswada wa Sheria ya Kurekebisha sheria mbali mbali za Ardhi nja mambo yanayohusiana na hayo Kusomwa Kwa Mara ya Kwanza.

Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa idhini yako sasa naomba Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Biashara Zanzibar Nam. 4 ya mwaka 1989 na Katika vifungu vya kuimarisha biashara Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo Kusomwa Kwa Mara Kwanza.

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa heshima na taadhima naomba sasa Mswada wa sheria wa kuanzisha Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara na mambo yanayohusiana na hayo Kusomwa Kwa Mara ya Kwanza.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, miswada hiyo imesomwa kwa mara ya kwanza na nategemea tumeipokea kwa ajili sasa ya kufanyiwa kazi na kamati zinazohusika. Ahsante sana, tunaendelea.

TAARIFA

Ndg. Katibu (BLW): Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa taarifa kwamba hapa ndio mwisho wa shughuli zetu kwa mujibu wa orodha ya shughuli za leo na kwa hatua basi naomba kutoa taarifa kwamba hapa ndio mwisho wa shughuli zilizopangwa, kwa ajili ya Mkutano wa 12 wa Baraza la Nane la Wawakilishi la Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mkuu wa Shughuli za Serikali ndani ya Baraza hili, naomba nichukue nafasi hii kusema mawili matatu ili akimaliza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais basi iwe ni mwisho wa shughuli zetu.

Kwanza kabisa nichukue nafasi hii Waheshimiwa Wajumbe kukushukuruni sana kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya kwa umoja wetu na kwa mashirikiano makubwa ambayo hatimaye tumefanikiwa kufanya shughuli zote ambazo zilikuwa zimepangwa katika mkutano huu hasa hasa bajeti kuu ya serikali na bajeti ya wizara mbali mbali. Lakini pia tumefanikiwa kwenda kwenye semina mbali mbali ambazo zilipangwa kwa kipindi cha mkutano mzima huu.

Waheshimiwa Wajumbe kazi hiyo nzuri imefanikiwa kwa sababu ya mashirikiano makubwa ambayo tumeonesha kati yetu. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambaye mara zote amekuwa yupo pamoja nasi katika kuona kwamba shughuli zetu hizi zinakwenda vizuri lakini pamoja na Mnadhimu wa Serikali Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini kwa ujumla Waheshimiwa Mawaziri mumeonesha upeo wenu wa mashirikiano katika kutekeleza shughuli zetu. Hoja zilikuwa ni nyingi zimetuchukua muda lakini ninachoshukuru zaidi ni kwamba hakuna aliyeripuka na hatimaye akapanda mori. Tulikwenda kwa utulivu kwa murua na hatimaye tukafanikisha shughuli hiyo zetu.

Kwa upande wa Waheshimiwa Wajumbe wengine kwa ujumla nao pia mlitupa mashirikiana makubwa sana katika kutekeleza shughuli hizo, tulijaribu kwa kiasi kikubwa kupokea hoja mbali mbali ili tuone kwamba serikali tunaisimamia vyema na kutoa maelekezo yanayofaa kabla hatujatoa idhini ya maombi ya makadirio mbali mbali ambayo yaliletwa mbele yetu kuwa ni sehemu ya matumizi pamoja na mapato kwa wizara mbali mbali.

Kazi hiyo nzuri isingefanikiwa kama si kwa mashirikiano makubwa sana ambayo wenzangu Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wawili wa Baraza walinipa muda wote wakati wa kufanya shughuli zetu hizo. Hapana shaka nisingemudu hata kidogo kufanya shughuli hizo peke yangu bila ya wao wakati wote walikuwa tayari ili kusaidia pale ambapo nilikuwa na dharura ama kwa sababu ya shughuli nyengine au wakati mwengine kama binadamu kutaka kupumzika kidogo.

Lakini utaratibu mzima huo wa shughuli zetu na mwenendo wote ulitengenezwa na kutaratibiwa vizuri na Katibu wa Baraza la Wawakilishi ndugu yetu Yahya Khamis Hamad, akishirikiana na wetendaji wenziwe na wafanyakazi wote walikuwa tayari kwa muda wote ili kuwahudumia Waheshimiwa Wajumbe kuona kwamba shughuli zetu za Mkutano huu wa 12 zinafanyika vizuri na kwa ufanisi mkubwa.

Vile vile ndugu zetu hawa waandishi wa habari waliokuwemo humu ndani na hasa watu wa kamera wakati wote wamekuwa wapo pamoja nasi. Nadiriki

kusema pengine kazi yao ilikuwa kubwa zaidi hata kuliko sisi na maneno hayo mliyasema nyinyi Waheshimiwa Wajumbe kwamba angalau Waheshimiwa Wajumbe tunapata kutoka toka kunyoosha miguu, lakini wao hawakupata nafasi hiyo, muda wote walikuwa ndani ya ukumbi na kuhakikisha kwamba wanaweza kuki-*cover* kikao chote kwa muda wote tangu tarehe 12/06/2013 hadi leo hii tarehe 06/08/2013. Kwa hivyo nawapongeza sana watu wetu wa kamera pamoja na waandishi wengine wote wa habari ambao walimekuwa wanashirikiana nasi katika shughuli zetu.

Pamoja na ndugu zetu wa tafsiri pale ambao na wao wamesaidia sana kwa wale watu ambao hawawezi kusikia na wakati mwengine hawawezi kusema. Wamesaidia sana kutoa tafsiri ya shughuli zote zilizokuwa zinaendelea hapa kwa muda wote bila ya kuchoka. Nachukua nafasi hii pia na wao kuwapongeza sana kwa shughuli hizo nzuri.

Mara hii sikusikia malalamiko kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe kama kuna watendaji wa serikali ambao walikuwa wanapaswa wawepo wakati wa shughuli zao kama walikuwa hawapo. Hata pale walikuwa wanahitajika wafike haraka sana basi walifanya hivyo kwa mfano watendaji wa Wizara ya Biashara walikuwa hawana habari kwamba shughuli yao inaanza lakini haraka sana walifika ili kuona kwamba waone kile kinachoendelea na wachukue nukta zote Waheshimiwa Wajumbe mlikuwa mnazisema katika maswali na hoja mbali mbali.

Waheshimiwa Wajumbe nimetaka niseme hayo ili Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akimaliza shughuli yake basi mimi tena nisiwe na maneno mengine ila kuahirisha Mkutano huu wa 12.

Naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo nikushukuruni tena kwa mashirikiano makubwa mliyotupa. Sasa naomba kwa heshima na taadhima nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. (*Makofi*)

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii adhimu kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kwa mara nyingine tena kukutana hapa katika mkutano huu wa 12 wa Baraza la Wawakilishi ambao unamalizika ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa mafanikio makubwa sana.

Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu kuendelea kuwa katika hali ya amani, utulivu, usalama na mshikamano, mambo ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mhe. Spika, naomba pia kutoa pongezi zangu za dhati kwako binafsi Mhe. Spika pamoja na wasaidizi wako wote, wakiwemo Mhe. Naibu Spika na Wahe. Wenyeviti wa Baraza kwa kuendelea kuliongoza Baraza letu kwa busara, hekma na ufanisi mkubwa kwa kufuata misingi ya kidemokrasia na Kanuni za Baraza.

Pia, napenda kuwapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati mbali mbali za Kudumu za Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wote wa Baraza hili Tukufu kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa hekma na uadilifu mkubwa.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati kiongozi wetu mpendwa, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake thabit na imara uliojaa hekma, busara na upeo mkubwa unaozingatia malengo na matarajio ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, sina budi pia kutoa shukrani nyingi kwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad kwa kumshauri na kumsaidia vyema Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuiongoza nchi yetu kwa misingi ya utawala bora. Vile vile, naomba kuwapongeza sana Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na watendaji wote wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao vyema kwa lengo la kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, aidha napenda kuwashukuru sana waandishi wa vyombo vyote vya habari. Sisi sote hapa ni mashuhuda jinsi waandishi wa habari katika Baraza walivyoweza kufuatilia kwa makini mwenendo mzima wa matukio mbali mbali ndani na nje ya Baraza, ikiwemo utoaji wa taarifa za hoja, michango na mijadala iliyojitokeza Barazani na kuwafikia wananchi wetu. Nachukua nafasi hii kuvipongeza na kuvishukuru sana vyombo hivyo kwa kutekeleza vyema jukumu lao kuwapasha habari za Baraza wananchi ipasavyo.

Natoa pongezi za pekee kwa wakalimani wa lugha ya alama kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kutafsiri mijadala kwa ishara ili kuwawezesha wananchi wetu wenye ulemavu wa kutokusikia kupata taarifa juu ya mijadala yetu ndani ya Baraza.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa naomba nizungumzie juu ya tukio la msiba uliotupata nchini kwetu hivi karibuni. Taifa letu lilipokea kwa mshituko na huzuni kubwa taarifa ya vifo vya wapiganaji wetu saba wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ambao wameuawa nchini Sudan baada ya

kuvamiwa na waasi wa Darfur katika harakati za kusaidia kuweka amani nchini humo. Vifo vya wapiganaji hao ni msiba mkubwa kwetu sote. Ni dhahiri kuwa wapiganaji wetu hao wameonesha ujasiri na moyo wa uzalendo mkubwa kwa wananchi wa Tanzania na kwa Bara la Afrika.

Ni ukweli usiopingika kuwa wapiganaji hao wamekufa kishujaa na nimefarajika sana kuona kwamba mazishi yao yamepewa heshima zote za Kitaifa. Katika tukio hilo la kuhuzunisha walikuwamo wanajeshi wawili kutoka Brigedi ya Nyuki ya Zanzibar ambao ni Sajenti Shaibu Shehe Othman na Koplo Mohammed Juma Ali. Naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kutoa salamu za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wote na nawaomba wawe na subra katika kipindi hiki kigumu cha huzuni na maombolezo, Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu pahala pema peponi, Amin.

MASUALA MUHIMU YALIYOJIRI NCHINI

Mhe. Spika, wakati serikali ipo katika hatua ya kutekeleza malengo ya maendeleo, hususan kutekeleza mikakati na sera ya matumizi na umiliki wa ardhi, juhudi kubwa zinaendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha ardhi tuliyonayo inatumiwa ipasavyo na inatoa tija kubwa zaidi. Lengo la mikakati na sera za ardhi ni kutatua kwa uadilifu migogoro ya ardhi inayojitokeza mara kwa mara hapa nchini.

Miongoni mwa hatua zinazoendelea kuchukuliwa kuhusiana na suala la migogoro ya ardhi ni zoezi linaloendelea la usajili wa ardhi na kuhakikisha kwamba ardhi yote ya Zanzibar inasajiliwa na taarifa zake zinawekwa katika daftari maalumu. Madhumuni ya zoezi hilo ni kuiwezesha serikali kupata taarifa sahihi za watu wote ambao wana haki ya matumizi ya ardhi. Pia, hatua hiyo itaiwezesha serikali kupanga matumizi mazuri ya ardhi pamoja na kuweka kumbukumbu sahihi za wamiliki wa ardhi hizo nchini.

Mhe. Spika, katika hatua nyengine ya kupunguza mrundikano wa kesi za ardhi, Serikali imepanga kuanzisha Mahakama za Ardhi katika kila Mkoa pamoja na kuongeza idadi ya Mahakimu wa Mahakama ya Ardhi Unguja na Pemba ili kurahisisha na kuharakisha mwenendo wa kesi za migogoro ya ardhi ambazo zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku.

Mhe. Spika, azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwa na miji ya kisasa yenye huduma za aina zote. Katika suala la upangaji wa miji na matumizi ya ardhi, serikali inaendelea na zoezi la utayarishaji wa *master plan* ya Mji wa Zanzibar na Mpango wa Mji wa Chake Chake. Lengo ni kuipanga upya miji hiyo ambapo suala la makaazi, biashara, viwanda na maeneo ya

michezo na mapumziko yamezingatiwa kwa kina kwani maeneo haya yote ni muhimu kwa uchumi na afya za wananchi wetu.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa wananchi na viongozi kufuata taratibu za usajili wa ardhi ili kuhakikisha tunakuwa na matumizi mazuri ya ardhi pamoja na kupata ufumbuzi wa kudumu wa migogoro ya ardhi inayojitokeza mara kwa mara. Lakini pia, ningependa kuwasihi watendaji wa Wizara ya Ardhi kutekeleza maagizo ya viongozi yenye nia ya kuleta suluhu katika migogoro ya ardhi inayojitokeza kwani wakati mwengine wanachukua muda mrefu kutekeleza maagizo hayo.

Mhe. Spika, kwa muda mrefu sasa Zanzibar imekuwa ikitumia chanzo kimoja cha umeme. Hali hii imepelekea kupata malalamiko kutoka kwa wananchi pale inapotokea hitilafu za kukosekana kwa umeme au kupanda kwa gharama za huduma hiyo muhimu. Kwa msingi huo, serikali imetoa kipaumbele katika kutafuta chanzo cha nishati mbadala ya uhakika badala ya kutegemea chanzo kimoja cha umeme.

Hivyo, kwa kupitia wizara inayohusika, serikali inaendelea na utafiti yakinifu wa kupata nishati mbadala. Tunatarajia baada ya utafiti huo, Zanzibar itaweza kupata chanzo chengine cha nishati mbadala na hatimae kuwekeza katika uzalishaji wa nishati hiyo. Mpaka hivi sasa wamejitokeza wawekezaji kadha walioonesha nia ya kuwekeza katika miradi ya umeme mbadala. Wapo wa kutumia *solar*, upepo, takataka na mawimbi ya bahari.

Nam702

IMESAHIHISHWA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: (anaendelea) wapo wa kutumia *solar*, wapo wa kutumia upepo, wapo wa kutumia takataka na wapo wa kutumia mawimbi ya bahari. Hivi sasa serikali inachunguza ni mradi wa aina gani utakuwa wa manufaa zaidi kwa nchi, kiuchumi na kimazingira.

Mhe. Spika, hivi sasa tunakabiliwa na changamoto nyingi za uharibifu wa mazingira na zaidi tatizo hilo limejitokeza kutokana na kuwepo kwa athari za mabadiliko ya tabianchi, maendeleo ya sekta ya utalii, ujenzi wa miundombinu na ukosefu wa miundombinu ya uondoaji wa taka pamoja na uingizaji wa bidhaa chakavu za elektroniki na mifuko ya plastiki.

Katika juhudi za kukabiliana na hali hiyo, serikali imechukua hatua za kuanzisha Sera mpya ya Mazingira ya mwaka 2013, Mkakati wa Zanzibar wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi, kuweka Kanuni za Usimamizi Endelevu wa Maliasili Zisizorejesheka pamoja na kufanya mapitio ya Sheria ya Mazingira Nam. 2 ya mwaka 1992.

Mhe. Spika, sambamba na hatua hizo, serikali imekamilisha muongozo ambao utaitaka kila taasisi kuwa na wajibu wa kutekeleza mipango yake kwa kuzingatia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Kwa kuzingatia umuhimu wa suala hilo, serikali inawashauri wananchi kupanda miti kwa wingi katika maeneo mbali mbali hasa miti ya matunda na mazao ya biashara. Naomba kuwatanabahisha wananchi kwamba serikali haitamvumilia mwananchi yeyote atayekwenda kinyume na taratibu za uhifadhi wa mazingira nchini kwa sababu kama hatukuwa waangalifu katika kuyalinda mazingira yetu, nchi yetu itaweza kupata majanga makubwa.

Mhe. Spika, katika muktadha wa kuhifadhi mazingira na kumlinda mtumiaji, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba serikali kupitia taasisi zinazohusika imeweza kuangamiza tani 700 za unga wa ngano mbovu ulioingizwa nchini kinyume na sheria. Naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru kwa dhati Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mashirikiano makubwa iliyotupa kufanikisha uangamizaji wa unga huo. *(Makofi).*

Katika kuhakikisha kuwa tunakuwa na mfumo madhubuti wa kusimamia ubora wa bidhaa nchini, serikali inaifanyia marekebisho Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2006 kwa lengo la kudhibiti uingizaji na utumiaji wa bidhaa hizo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawaagiza wafanyabiashara wote kuwa makini wakati wa kuingiza nchini bidhaa zao zisiwe zilizopitwa au zinazokaribia kupitwa na muda wake wa matumizi pamoja na bidhaa mbovu. Serikali itawachukulia hatua kali wafanyabiashara wote watakaokwenda kinyume na agizo hili, kwani ni wajibu wa serikali kuwalinda wananchi wasile vyakula vibovu vitakavyoweza kuwaletea madhara.

Mhe. Spika, katika kufanikisha utekelezaji mzuri wa masuala ya viwango vya bidhaa, Serikali inaijengea uwezo Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (*Zanzibar Beurau of Standards – ZBS*), ili iweze kuweka viwango vya bidhaa zinazoingizwa na kutengenezwa nchini. Azma hiyo inatokana na umuhimu wa kuepusha nchi yetu kugeuzwa kuwa jaa la kutupia bidhaa mbovu na zisizo na viwango na kulinda afya za wananchi wetu.

Wizara ya Biashara inaagizwa kuona umuhimu wa kuzikagua bidhaa kabla ya kuingizwa nchini, kwani kumekuwepo na malalamiko kuwa Zanzibar ni njia ya kupitisha bidhaa mbovu. Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (*ZBS*) inashauriwa kufungua ofisi nje ya nchi ili kuzikagua bidhaa zinazotaka kuingizwa nchini kabla ya kuingizwa nchini bidhaa hizo. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kuhusu suala la kuendeleza zoezi la Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivi sasa jamii imeshaunda Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na hatua za kukusanya maoni kupitia Mabaraza hayo inaendelea. Napenda kuwapongeza Wajumbe wote wanaowakilisha Mabaraza hayo kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwasilisha mawazo yao kwa amani na utulivu.

Hilo ni jambo la msingi sana katika kuhakikisha kuwa Wazanzibari wanawasilisha maoni yao ya Kikatiba kwa kufuata taratibu zilizowekwa kwa misingi ya demokrasia. Matarajio yetu kwamba ushiriki wa wananchi kupitia Mabaraza hayo utakuwa na mafanikio na hatimaye tutaweza kupata Katiba ambayo itakuwa na maslahi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa nchi yetu na wananchi wake. Hivyo, wananchi wanaombwa kutoa maoni yao kwa uhuru na uwazi bila ya woga.

Mhe. Spika, katika hatua nyengine zinazochukuliwa kuimarisha demokrasia na utawala bora nchini, serikali inaendelea kuratibu vyema zoezi la uhakiki wa daftari la kudumu la wapiga kura kupitia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (*ZEC*). Lengo la zoezi hilo ni kuwaandikisha wale wote wanaostahiki na kuwatoa wale ambao hawastahiki. Hili ni zoezi muhimu kwa maslahi ya kisiasa kwa wananchi wetu. Napenda kutoa wito kwa wananchi wote kushiriki kwa kikamilifu katika zoezi hilo.

Katika kufanikisha zoezi hili kwa amani na utulivu, nawasihi wananchi wote kufuata sheria na taratibu za uandikishaji zilizowekwa ikiwemo kuwa na ithibati zote zinazohitajika ili kuweza kuandikishwa bila ya bughudha. Wananchi wanaonywa kutowafanyia hila au vurugu wananchi wenzao ili kuwazuia wasijiandikishe. Hilo ni kosa la jinai na mtu atakayebainika kufanya hivyo atachukuliwa hatua za kisheria.

Mhe. Spika, ni jambo la faraja kuona kuwa sekta ya uvuvi imezidi kuimarika kutokana na kuongezeka kwa shughuli za uvuvi wa baharini na pia wananchi wengi wameanza kufuga samaki na mazao mengine ya baharini. Mafanikio makubwa yameweza kupatikana hasa katika kisiwa cha Pemba. Uchambuzi wa takwimu umeonesha kwamba katika kipindi cha mwaka 2012/2013 sekta ya uvuvi imepata mafanikio makubwa matatu yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza, idadi ya samaki wanaovuliwa imeongezeka kutoka tani milioni 28.8 hadi 29.4, sawa na ongezeko la tani 651 ambayo ni asilimia 2.3. Pili, wingi wa samaki wanaovuliwa umefikia jumla ya tani 9.8 kwa mwaka ambapo Pemba imevuna tani 7.7 na Unguja tani 2.1 kwa mwaka 2012/2013. Tatu, mafanikio makubwa katika zao la mwani kutoka tani 13 elfu mwaka 2011 mpaka tani 15 elfu mwaka 2013 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.

Mhe. Spika, kwa jumla shughuli zote za kilimo cha mwani, uvuvi wa baharini na samaki wa kufuga zimeweza kusaidia kuongeza kipato cha wananchi sambamba na malengo ya mpango wa pili wa kupunguza umaskini (MKUZA II) pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2010/2015. Katika kuendelea kuyalinda mazalio ya samaki, tunawasihi wavuvi kuacha uvuvi haramu, kwani uvuvi haramu unaweza kusabibisha uharibifu wa mazalia ya samaki na hivyo kupunguza idadi ya samaki baharini. Wavuvi wakumbuke kuwa wakivua leo, waweke akiba ili waweze kuvua na kesho. *(Makofi).*

Mhe. Spika, hali ya sekta ya mifugo nayo imeanza kutoa matumaini yenye kutia moyo. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kuimarika kwa utoaji wa huduma za uzalishaji na utibabu wa mifugo. Pia kujengwa kwa mitambo mipya ya gesi asilia (*biogas*) kumi na moja (11), Unguja minane na Pemba mitatu. Kukamilika kwa ujenzi wa mitambo hiyo kumepelekea kuwa na mitambo 24 kwa Unguja na Pemba iliyokwisha kujengwa. *(Makofi).*

Mhe. Spika, katika juhudi za kuwawezesha wananchi kiuchumi serikali imetoa jumla ya mikopo 193 yenye thamani ya shilingi milioni 156 kwa kupitia Mfuko wa Kujitegemea. Aidha, serikali imetoa shilingi milioni 303 kwa vyama vya ushirika na vikundi vya wajasiriamali 199 kwa kupitia Mfuko wa Zaka.

Mhe. Spika, katika kuimarisha uratibu wa utoaji wa mikopo midogo midogo, serikali imeanzisha mtandao wa taasisi zinazotoa huduma za fedha kwa wajasiriamali wadogo. Mtandao huo unajumuisha taasisi mbali mbali zikiwemo *WEDTF*, *YOSEFO*, Benki ya *CRDB*, Changamoto, Meli-nne *SACCOS* na Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar.

Lengo la mtandao huo ni kubadilishana taarifa za wakopaji ili kuweza kutathmini idadi ya watu wanaofikiwa kwa huduma za mikopo na pia kuimarisha mashirikiano katika huduma zao. Hatua hii inasaidia kubainisha thamani na aina ya mikopo ambayo hutolewa na taasisi mbali mbali kwa wajasiriamali na namna mikopo hiyo inavyowasaidia wajasiriamali hao kuendesha maisha yao na kujikomboa kutoka kwenye umaskini.

Mhe. Spika, katika kuimarisha usafiri wa baharini mnamo tarehe 10 Julai, 2013 serikali imetiliana saini mkataba wa ujenzi wa meli ya abiria na mizigo na kampuni ya *Daewoo* ya Korea ya Kusini. Meli hiyo ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua abiria 1200 katika daraja tatu tofauti na uwezo wa kubeba mizigo yenye uzito wa tani 200, itakamilika ujenzi wake baada ya miezi 23 kuanzia Julai mwaka huu.

Mhe. Spika, hatua hii imekwenda sambamba na ukarabati wa jengo jipya la abiria katika eneo la bandarini kwa mashirikiano na mwekezaji wa kizalendo S.S. Bakhresa wa Kampuni ya *Azam Marine*. Uzinduzi wa mradi huu umefanyika rasmi tarehe 8 Julai, 2013. Serikali inatoa shukurani za dhati kwa uongozi wa Kampuni ya *Azam Marine* kwa mchango wao mkubwa katika kusaidia maendeleo ya shughuli za usafiri kwa kuwaondolea bughdha wasafiri.

Mhe. Spika, tarehe 12 Januari, 2014, nchi yetu itaadhimisha miaka 50 ya mapinduzi matukufu ya Zanzibar. Maadhimisho hayo yanatarajiwa kuwa ya aina yake na yatazinduliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein tarehe 15 Agosti, 2013 kwa lengo la kufanikisha sherehe za maadhimisho hayo, serikali inatoa wito maalumu kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kwa pamoja na sekta binafsi kushirikiana na serikali ili kuzifanya sherehe hizo kuwa za kihistoria pamoja na kuzipa hadhi ya juu na ya kipekee.

Sherehe hizo zitajumuisha mafanikio ya utekelezaji wa sekta zote za uzalishaji na utoaji wa huduma kwa kuonesha maendeleo yao ya miaka 50 ya mapinduzi. Madhumuni ya kufanya sherehe hizo yanatokana na haja ya wananchi wa Zanzibar kuelewa na kutathmini wapi tulipotoka, tulipo sasa na wapi tunapokusudia kwenda kwa mtazamo wa kuinua hali za maisha ya wananchi walio wengi na kuharakisha maendeleo ya nchi kwa jumla.

Mhe. Spika, katika mkutano huu wa 12 wa Baraza lako Tukufu, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza walijadili na kupitisha Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2013/2014. Aidha, Waheshimiwa Mawaziri wamewasilisha Miswada miwili ya sheria ambayo ina umuhimu mkubwa kwa ustawi na maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, Mswada wa kwanza uliojadiliwa ni Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Madhumuni ya mswada huo ni kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali na kuweka utaratibu mzuri wa udhibiti

ukusanyaji wa mapato. Mhe. Spika, Mswada wa Pili ni Mswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma (*Appropriation Bill*).

Mhe. Spika, katika kikao hiki cha 12 Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara zote waliwasilisha hotuba za mapato na matumizi za Wizara zao kwa mwaka fedha 2013/2014, na Waheshimiwa Wajumbe walipata nafasi ya kuzijadili, kuzichangia kwa uangalifu, umakini na uadilifu mkubwa na hatimae kuzipitisha. Waheshimiwa Wajumbe walipata nafasi ya kuhoji kwa yale mambo ambayo walihisi hayakuwa bayana na yalihitaji ufafanuzi na Waheshimiwa Mawaziri kwa mujibu wa Kanuni za Baraza walitoa ufafanuzi unaostahiki na hatimaye Wajumbe walizipitisha bajeti za mwaka huu, ingawa baadhi ya Bajeti hizo zilipita kwa mbinde. *(Makofi).*

Hii imeonesha umakini mkubwa waliokuwa nao Wajumbe wa Baraza. Naomba kusisitiza kwamba baada ya Baraza kufanya kazi kubwa ya kuzichambua, kuzihakiki na kutoa mapendekezo katika Bajeti za Wizara mbali mbali, uongozi wa wizara zote kuwa makini katika matumizi na usimamizi kwa mujibu wa malengo na taratibu za matumizi ya fedha. Waheshimiwa Mawaziri na Makatibu Wakuu wanaombwa kusimamia kwa makini matumizi ya fedha za wizara zao zilizoidhinishwa na Baraza hili.

Mhe. Spika, baadhi ya Wajumbe katika uchangiaji wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi walihoji juu ya uagizaji wa kuku kutoka nje ya nchi. Mjadala mrefu ulitokana na wasi wasi wa baadhi ya Wajumbe hao kuwa uingizaji wa bidhaa hiyo utadhoofisha soko kwa wafugaji wa ndani na hatimaye kuwakosesha kipato wafugaji hao. Ukweli dhana hiyo sio kweli, kwani serikali inazingatia sana hali za wananchi wake si wafugaji au wafanyabiashara pekee. Kabla ya serikali kufanya uamuzi huu, ililitafakari kwa kina suala hili na hatimae kufanya uamuzi huo baada ya kuona kuwa haukuwa na madhara kwa wafugaji wetu. *(Makofi).*

Hata hivyo, naomba kueleza kuwa serikali kwa muda mrefu hapo nyuma iliamua kuchukua hatua za kuimarisha ushindani wa kibiashara. Lakini tatizo kubwa linalojitokeza ni kwamba mahitaji ya soko la kuku Zanzibar ni kubwa. Kwa hivyo, kwa kipindi hiki si vyema kuchukua hatua yoyote ya kubana uingizaji wa kuku kutoka nje hadi pale soko la ndani litakapoweza kujitosheleza. Kwani tukichukua hatua hiyo ghafla tunaweza kuhatarisha mahitaji halisi ya biashara katika sekta nyengine hasa sekta ya utalii nchini.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wasilichukulie suala hili kuwa sawa na wenzetu wa Tanzania Bara. Tukijilinganisha na wao kwa hali zetu tutakosea kwani sababu zao ni tofauti na zetu kwa sababu:-

a) Wenzetu Tanzania Bara wana wafugaji wengi wanaozalisha kwa viwango vinavyotakiwa.

b) Waliamua kuzuia uletaji wa kuku pamoja na mambo mengine kwa sababu ya maradhi. Mambo ambayo uletaji wa kuku wetu huwa yanazingatiwa kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anaendelea kutoa hotuba ya kufunga mkutano huu. Naomba tuzingatie hotuba hiyo na tumsikilize. Tuendelee.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais:

c) Wananchi wetu wengi hawawezi kumudu bei za kuku hapa nchini. Hii ni kutokana na gharama kubwa mno za uzalishaji.

Kwa maana hiyo serikali haikupuuza ushauri wa baadhi ya Wajumbe wa Baraza, bali itaendelea kufanya utafiti wa hali halisi ya biashara hiyo ili tufaidike sote wafugaji na walaji pia. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kwa kuelewa wasi wasi wa wafugaji wa kuku wa ndani, serikali itaendelea kuangalia mwenendo mzima wa uzalishaji na uagizaji wa kuku ili kuhakikisha kuwa wafugaji wa ndani hawaathiriwi na suala hilo, kama Baraza lilivyoelekeza. Serikali itawasaidia wafugaji wetu ili wazalishe zaidi ili tuweze kupunguza uagizaji kidogo kidogo hadi pale tutakapojitosheleza kwa ukamilifu. *(Makofi).*

Mhe. Spika, baada ya kukamilisha kazi za awali za mradi wa *e-government* ikiwemo kutandika mkonga wa "*fibre optic*", Serikali imeendelea na kazi za kuimarisha teknolojia ya habari na mawasiliano. Kutokana na umuhimu wa suala hilo, hata Wajumbe wa Baraza walichangia sana juu ya haja ya kukamilisha mradi wa *e-government*. Hivyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwahakikishia Wajumbe pamoja na wananchi kuwa serikali imekusudia kwa dhati kufanikisha mradi huu haraka iwezekanavyo. *(Makofi).*

Madhumuni hasa ya mradi huu yanalenga katika kuendesha na kusimamia matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika sekta ya utumishi wa umma, ili kuhakikisha kuwa usimamizi wa kumbukumbu za eletroniki pamoja na teknolojia ya habari na mawasiliano unatumika katika kuimarisha huduma za utawala bora. Mradi huu utaanzisha mfumo wa pamoja utakaotumiwa na taasisi zote za umma pamoja na kuweka mazingira mazuri ya utekelezaji wa jumla kwa mujibu wa dhana ya kuimarisha utoaji wa huduma za serikali zilizounganishwa ki-eletroniki.

Mhe. Spika, serikali ya mtandao kwa muda huu tulionao ni kitu cha lazima. Kwa msingi huo, naomba nitoe tahadhari kuwa mafanikio ya mradi huu yatafikiwa sambamba na jamii kuweza kutumia vyema teknolojia ya kompyuta. Hatua hii itapelekea haja ya viongozi, watumishi wa serikali pamoja na wananchi kuchukua juhudi za makusudi kujifunza kutumia kompyuta. Tukizingatia kwamba teknolojia hii inakuwa kwa haraka mno na tusisite kujifunza hivi sasa kwani tukijifunza baadae tutakuwa tumechelewa mno na hivyo tutapitwa na wakati.

Mhe. Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako Tukufu kuwa serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha sekta za utoaji huduma, ikiwemo sekta za maji safi na salama, afya, elimu na miundombinu. Kwa upande wa uzalishaji, serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa kuimarisha sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, viwanda vidogo vidogo, utalii na biashara nchini. Lengo kuu la juhudi hizi zinazochukuliwa na serikali ni kukuza uchumi na kupunguza umaskini katika nchi yetu.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kusisitiza mambo yafuatayo:

Kwanza, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wajue kuwa tumemaliza Mkutano wa Baraza hili la kumi na mbili na hivyo ni vyema wakarudi katika majimbo yao ili kushirikiana na wananchi wao katika harakati za kuleta maendeleo kwa nia ya kuimarisha maelewano baina ya wananchi na Wawakilishi wao.

Pili, katika suala la ardhi tunawaomba wananchi na viongozi kufuata taratibu zilizowekwa katika suala la uhifadhi wa mazingira, umiliki na matumizi mazuri ya ardhi, pamoja na viongozi wa ngazi zote kuacha kabisa tabia potofu zinazochangia ongezeko la migogoro ya ardhi nchini.

Tatu, kwa upande wa watendaji wakuu wa serikali tunasisitiza uwajibikaji kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na kuhakikisha utekelezaji wa malengo ya bajeti unaendeshwa kwa misingi ya uadilifu kama ilivyosisitizwa katika mkutano huu wa kumi na mbili kwa azma ya kufikia matarajio ya wizara zetu.

Agizo hili liende sambamba na utekelezaji wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma na tuepukane kabisa na mtindo wa utekelezaji wa kufanya kazi kwa kutumia uzoefu (*business as usual).* Serikali itaendelea kuliunga mkono Baraza la Wawakilishi katika juhudi zake za kuwafichua watendaji wabadhirifu na wabinafsi na kuwachukulia hatua wanazostahiki. Lakini kuifanikisha kazi hii lazima sote tuwe na sauti moja ya kuwafichua na sio

wengine kuwa mawakili wa wafichuliwa. Hata wakipenda kufanya hivyo basi waujue ukweli kuwa hicho wanachokitetea na sio kuwapotosha wananchi. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu, ningependa nieleze machache kuhusu suala zima la amani na utulivu katika nchi yetu. Nalisema hili kwa sababu kila mmoja wetu naamini anafahamu umuhimu wa amani kwa nchi yoyote ile sio hapa nyumbani tu. Kwa maana hiyo ndio sababu mataifa mbali mbali huwa makali wakati nchi zao zinapohatarishiwa utulivu na amani yao.

Hivi karibuni amejitokeza kiongozi wa kidini kutoka nje ya visiwa hivi na kuanza kupita Misikitini kwa lengo la kutoa mihadhara ya uchochezi dhidi ya serikali na viongozi wake, mihadhara ambayo ilikuwa ya kuwapotosha wananchi. Kitendo hicho kwa kweli ni cha kusikitisha na hakikuwa cha kiungwana na kinakwenda kinyume na maadili ya dini yenyewe ya Kiislamu, licha ya kuhatarisha amani na utulivu uliopo.

Lazima ifahamike wazi kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika suala la kudumisha amani haina stahamala wala muhali. Haitosita kuchukua hatua kali kwa mujibu wa sheria za nchi kwa kikundi au mtu yeyote atakayeonekana kujiingiza kwa njia moja au nyengine katika kuchezea amani yetu. Serikali itailinda amani ya nchi na wananchi wake kwa gharama yoyote ile.

Mhe. Spika, Zanzibar haina mgongano wowote wa dini wala waumini wa dini zozote, endapo viongozi na waumini wake watafanya ibada zao kwa kufuata sheria na taratibu za nchi zilizowekwa. Kwa mnasaba huo, serikali haitakubali kuona kiongozi wa dini kufanya mahubiri yanayoelekeza sura za uchochezi zinazopelekea kuondoa utulivu badala ya mshikamano wa raia wote.

Hivyo, serikali inalaani vitendo vya mahubiri ya aina hiyo hususan kitendo cha kiongozi huyo kufanya mihadhara ndani ya Misikiti kadhaa hapa nchini kwa lengo la uchochezi. Katu hakitavumiliwa na serikali haitahofu kutupiwa lawama kwa hatua itakazochukua dhidi ya watu wa aina hiyo. Hii ni kwa sababu sote tunafahamu kuwa amani na utulivu tulionao umepatikana kwa gharama kubwa. Hapa ningependa kuwaasa wananchi wasiwaunge mkono viongozi wa aina hiyo, kwani hawaitakii mema nchi yetu na wanataka kuturejesha nyuma katika hali ya uadui, uhasama miongoni mwa jamii yetu.

Mhe. Spika, kitendo cha muhubiri huyo kuleta uchochezi nchini mwetu kupitia Misikitini ni kutusababishia kutokea kwa vurugu nchini ambapo hatimaye ni sisi wenyewe ndio tutakaoumizana. Muhubiri huyo amekaanga mbuyu na kuwaachia wenye meno watafune. Zikitokea vurugu na ukosefu wa

amani nchini, tutakaoumizana ni sisi, yeye atakuwa hayupo wala mkewe na watoto wake. Nawasihi sana wananchi wasiyafuate mahubiri hayo. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nimepata habari kuwa kuna kikundi cha watu kimeanzisha utaratibu wa kupita katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba na kuwahoji wananchi kuwa ni wafuasi wa Chama gani CCM au CUF? Wamekuwa kama wanajaribu kufanya sensa ya kujua katika maeneo hayo kuna wanachama wangapi wa CCM na wangapi wa CUF.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuwaeleza wananchi wote kwamba serikali haina habari na zoezi hilo na wala haijatoa agizo la kufanyika kwa sensa hiyo. Hivyo, ninawaomba wananchi wasikubali kushiriki katika zoezi hilo ambalo halina baraka za serikali. Aidha, ningependa kukionya kikundi hicho kuliacha zoezi hili mara moja kwa sababu serikali haiendeshi sensa ya aina hiyo.

Mhe. Spika, katika suala hili ningependa kuwaomba Masheha wote, Unguja na Pemba kulifuatilia suala hilo kwa karibu na kuhakikisha kuwa zoezi hilo halifanyiki katika maeneo yao.

Mhe. Spika, katika mikutano kadhaa ya Baraza na hasa katika Mkutano huu wa Bajeti, jambo moja limekuwa likijitokeza sana, nalo ni matumizi ya taarifa na nyaraka za serikali ambazo baadhi yao ni za siri.

Kuhusiana na suala hili, kwanza nitangulie kueleza wazi kuwa serikali inaelewa na kuthamini kuwa msingi mmoja wa utawala bora ni uwazi.

Lakini naamini kuwa Waheshimiwa Wajumbe wote watakubaliana na mimi kuwa uwazi hauna maana kuwa hakuna utaratibu tena wa kupata taarifa na nyaraka za siri za serikali, na wala haina maana kuwa ni ruhusa kwa kila mwenye taarifa ya serikali au hata taarifa za mtu binafsi azisambaze kwa kadri apendavyo yeye, kwani kwa upande wa pili, moja ya msingi mkuu wa haki za binadamu ni haki ya faragha. Tumeshuhudia mara kadhaa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wakilalamika na kuwa wakati kwa taarifa zao binafsi kama zile za maslahi yao kuwekwa hadharani bila ya ridhaa zao.

Hivyo, naomba kutanabahisha kuwa kwanza kwa mujibu wa Sheria ya Kinga, Haki na Fursa ya Baraza la Wawakilishi Nam. 4 ya mwaka 2007, hasa kifungu cha 9 inaelezwa wazi kuwa ni haki ya Wajumbe kupata taarifa kutoka serikalini ilimradi tu taarifa hizo hazizuiliki kutolewa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 19 cha Sheria hiyo.

Hata hivyo, kifungu chenyewe cha 9 cha Sheria hiyo ya Kinga, Haki na Fursa za Baraza kinaeleza wazi kuwa Wajumbe wana haki ya kupata taarifa kwa kufuata Sheria na Taratibu zilizowekwa na Sheria yenyewe. Sheria nyengine za nchi na taratibu za Serikali za kupata taarifa. Miongoni mwa taratibu zilizowekwa na Sheria ya Kinga ni kwa taarifa kutolewa na Ofisa Muhusika kwa Baraza au kwa Kamati.

Aidha, kama Mjumbe anataka taarifa kutoka katika Taasisi ya Umma na kama taarifa hizo si za matumizi ya jumla ya umma, utaratibu uliopo ni kwa kupitia Ofisi ya Baraza. Mbali ya Sheria hiyo ya Kinga, kuweka taratibu nilizoeleza, naomba niwatanabahishe watumishi na watendaji wa taasisi za umma kuwa Sheria ya Siri za Serikali Nam. 5 ya mwaka 1983, chini ya kifungu cha 5 cha Sheria hiyo imeweka bayana kuwa ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kutoa taarifa za serikali ambazo ama amekabidhiwa au amezipata kwa sababu ya kazi au wadhifa wake kwa mtu asiyehusika. Adhabu ya kosa hilo ni kifungo kisichozidi miaka kumi na mbili bila ya faini.

Mhe. Spika, sio nia wala madhumuni ya serikali kuficha au kuzuia taarifa za uovu wowote unaofanywa na mtendaji yeyote wa serikali bali inachosisitiza kufuatwa kwa taratibu. Serikali inaamini kuwa sheria na taratibu ziliopo kwa Waheshimiwa Wajumbe kupata taarifa wanazohitaji, zinatoa fursa ya kutosha kufanya hivyo kihalali bila ya kuvunja sheria wala taratibu ziliopo. Bila ya kufuata taratibu yatajitokeza mambo kadhaa kama tulivyoanza kuyaona. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na taarifa kutolewa nusu nusu au za upande mmoja, ilimradi mjumbe ajenge hoja anayopenda yeye na hivyo kuwapotosha Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa jumla. Aidha, baadhi ya taarifa zinapotolewa upande mmoja zinahatarisha maisha na usalama wa baadhi ya watendaji kwa kuonesha kama kwamba wao ndio waliotoa uamuzi wakati wanafanya hivyo katika kutekeleza majukumu ya kazi zao.

Mhe. Spika, katika mkutano huu tunaouahirisha leo, jumla ya maswali 104 ya msingi na maswali 246 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wawakilishi na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri husika. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuja na maswali mazuri yenye lengo la kujenga zaidi na kuimarisha uwajibikaji wa watendaji wa serikali. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa majibu yao ya kina ambayo hatimaye yaliwaridhisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu. *(Makofi).*

Mhe. Spika, ikiwa tunaendelea kutekeleza ibada ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani, naomba tuendelee kuimarisha amani na utulivu iliyopo nchini kwetu ili tuweze kunufaika na neema alizotujalia Mwenyezi Mungu pamoja na kupata fadhila za mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kwa kuwa hapatakuwa

na kikao chengine cha Baraza kwa kipindi hiki cha karibu, naomba pia kuchukua nafasi hii kutoa mkono wa Idd-el–Fitri kwenu Wajumbe wa Baraza hili Tukufu na wananchi kwa jumla. Nakutakieni kila la kheri na baraka katika Siku-kuu hii adhimu ya Idd-el- Fitri. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, Wajumbe wa Baraza lako, watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza, waandishi wa habari na wananchi wote kwa mashirikiano yao makubwa katika kuliendesha Baraza letu kwa mafanikio. *(Makof).*

Matarajio yetu kwamba wananchi wataendelea kuwa karibu nasi katika kuimarisha demokrasia na utawala bora pamoja na maendeleo ya taifa letu. Nawatakia safari njema na ya salama Waheshimiwa Wajumbe wote ya kurejea majimboni mwao. *(Makofi).*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja ya kuliahirisha Baraza lako Tukufu hadi siku ya Jumatano, tarehe 9 Oktoba, 2013 saa 3.00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa.
Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa makofi mengi muliyompa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kutokana na hotuba nzuri aliyoitoa mbele yetu. Vile vile nichukue nafasi kumshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa niaba yenu Waheshimiwa Wajumbe, kwa hotuba hiyo ambayo ametuelekeza masuala mengi yanayofaa kwa ajili yetu na wananchi wetu.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijawahoji nataka niseme masuala mawili. Nimepokea maombi kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe tofauti na kuna maombi matatu au manne hivi ambayo yana muelekeo mzuri sana. Kwa kuwa tumekaa kwenye Mkutano huu wa Kumi na Mbili kwa muda mrefu karibu kidogo miezi miwili, basi hapana shaka kama binadamu inawezekana tumekoseana hapa na pale na wala si jambo jema kuondoka humu ndani ikawa mmoja anadonge dhidi ya mwenzake au kati yetu.

Kwa hivyo, nimeombwa nitoe taarifa na maombi kwenu Waheshimiwa Wajumbe kwamba inafaa sote hapa na pale kwa namna moja au nyengine tusameheane sana kutokana na mikwaruzo kwaruzo ambayo pengine imetokezea kupitia ama shughuli zetu hizi au kwa namna yoyote nyengine ingeweza kutokezea binadamu wanapokuwa pamoja.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba kwa niaba yenu niseme tu kwamba nawashukuru waliotoa mawazo hayo. Kwa hivyo, ninakuombeni basi kila mmoja wetu sote Waheshimiwa Wajumbe, watendaji pamoja na wenzetu wa habari nao pia wametuomba radhi hivyo ili tuweze kuwa pamoja na tusameheane yaliyopita yamepita, ili kutusafishia nia pamoja na saumu zetu ziweze kutakabaliwa vizuri na Mwenyezi Mungu. Kwa kweli nashukuru sana na makofi hayo inaonesha kwamba tunaafiki jambo hilo. *(Makofi)*

Vile vile nimeombwa na Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kwamba niwatangazie wale Waheshimiwa Wanamichezo wanawake, kwamba mazoezi yale yataanza siku ya siku kuu tatu na hapana shaka ni matayarisho ya kwenda Arusha pia kuleta afya kwa wanamichezo hao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuahirisha mkutano huu hadi tarehe 9/10/2013 saa 3:00 za asubuhi wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo na kukubaliana pamoja na kusameheana. Sasa naomba kuahirisha mkutano huu hadi siku ya Jumatano tarehe 09/10/2013 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 4:12 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi tarehe 09/10/2013 saa 3:00 za asubuhi)

WIMBO WA TAIFA